	AWAMU YA PILI MWEZESHAJI DR. G. NDUNGURU	
7.00-7.45	ULIMAJI NA UTUNZAJI WA MLONGE	E. SHUNDA
7.45-8.30	ULIMAJI NA UTUNZAJI WA ALOE VERA	Z.MBWAMBO
8.30-9.30	KUTEMBELEA SHAMBA NA SOLAR DRYER	E.SHUNDA NA DR.E.KAYOMBO
9.45-10.00	MAJADILIANO KWA UJUMLA NA MTAZAMO WA MBELE	WOTE
10.00-10.30	KUFUNGA SEMINA NA KIBURUDISHO	DIRECTOR NA MGENI MWALIKWA

HOTUBA YA UFUNGUZI WA WARSHA YA WADAU WAENDELEZAJI WA MADAWA YA MITI KAMA CHANZO CHA LISHE NA VIRUTUBISHO KATIKA WILAYA YA KIBAHA, TAREHE 22/05/2006.

MHESHIMIWA C. ISHENGOMA; MKUU WA MKOA WA PWANI

Mkurugenzi, Taasisi ya Madawa ya Asilia, Chuo Kikuu Kishiriki cha Sayansi za Tiba Muhimbili, viongozi Wilaya ya Kibaha, Wadau waendelelezaji wa dawa za miti na dawa asili, na washiriki wengine wa warsha hii.

Kwa niaba yangu, na kwa niaba ya wakazi wote wa Mkoa wa Pwani, napenda kuwakaribisha nyote hapa Kibaha, baada ya safari zenu ndefu kutoka huko vijijini na Dar es Salaam. Ninafahamu kuwa wengi wenu hamkai hapa karibu, pia ninafahamu wengine wametoka Dodoma, hivyo inabidi niwapongeze kwa juhudi kubwa mliyoifanya ili kuweza kuhudhuria katika warsha hii. Ninafahamu vilevile kuwa kutokana na barabara zetu kuharibiwa na mvua, inawezekana hata usafiri kutoka huko vijijini kwenu ulikuwa wa shida.

Ndugu washiriki wa warsha hii, mimi nimefahamishwa kwamba, warsha hii inalenga katika kubadilishana uzoefu kuhusu njia mbadala ya kupambana na janga hili la UKIMWI. Sote tunaelewa kwamba maambuzi ya UKIMWI katika Tanzania bado yanaendelea, na dawa ya kutibu bado haijapatikana. Ugonjwa huu hauna mipaka kwa vile unashambulia jamii za aina zote. Dunia nzima inakiri kwamba, ugonjwa huu hauna tiba kwa sasa na uwezekano wa kupata tiba bado uko mbali sana.

Ndugu washiriki, serikali yetu inajitahidi sana kutafuta njia mbalimbali za kupambana na tatizo hili la UKIMWI. Serikali inanunua dawa za kurefusha maisha ya waathika, kuhamasisha wananchi kupima afya zao pamoja na kutoa elimu kwa umma kuhusu athari za ugonjwa huu na jinsi ya kuepukana nao. Mafanikio yake bado yamekuwa kidogo sana na wananchi bado wanaendelea kuteketea. Ifahamike vilevile ya kuwa serikali haina uwezo wa kumpatia kila mwathirika mahitaji yake yote, ikiwa ni pamoja na lishe bora na dawa za kurefusha maisha. Ni wajibu wa wananchi wenyewe kutafuta njia na mbinu mbadala za kujisaidia, ikiwa ni pamoja na kutumia tiba na lishe zao za asili. Hatua ya serikali kusambaza dawa za kuongeza maisha ni ya kupongezwa. Hata hivyo dawa hizi zingeweza kumsadia zaidi mgonjwa wa UKIMWI kama zitaendana na uboreshaji wa lishe yake.

Ndugu wana warsha, mimi nimeelezwa kuwa warsha hii inalenga katika kuwaelimisha washiriki kuhusu umuhimu wa lishe zitokanazo na miti dawa katika kurefusha maisha ya waathirika wa UKIMWI.Vile vile nimeambiwa kuwa kwa kiwango kikubwa washiki watajifunza kuhusu matumizi ya tiba mbadala katika kutibu magonjwa mbalimbali yanayomwandama mwathirika wa UKIMWI kwa kutumia rasilimali zetu za misitu. Nimeambiwa kwamba, washiriki watajifunza jinsi ya kukuza mimea aina ya Mlonge, Rosella na Aloe vera na matumizi yake katika kutibu magonjwa mabalimbali kama vile shinikizo la damu, saratani,

kisukari na kupunguza makali ya UKIMWI.

Ndugu washiriki wa warsha hii, semina hii inafanyika wakati mwafaka kwa vile inalenga pia katika kuboresha mazingira yetu ambayo yanaelekea kuwa janga kwa sababu ya miti kukatwa ovyo. Mimi nina imani kabisa kuwa miti hiyo ikipandwa na kutunzwa vizuri itaweza kuhifadhi bianwai na hivi kuweka ikolojia nzima katika hali nzuri. Sina wasiwasi kuwa miti hii inaweza ikakua vizuri na kutoa bidhaa ambazo mkulima anaweza kuuza na kujipatia kipato kizuri na hivyo kuondokana na umaskini, ikiwa ni mchango wa ziada ukijumuishwa na manufaa ya moja kwa moja ya kujipatia lishe mbadala.

Ndugu zangu, mafanikio yote ya mradi huu yatategemea ni jinsi gani mtakavyoweza kushirikiana baina yenu, na taasisi nyingine. Mkakati huu ukiimarishwa vizuri utachangia katika kukuza kipato chenu kwa vile inategemewa kuwa mazao ya hii miti yataweza kuwekwa kenye vipakiti na kuuzwa sehemu mbali mbali hapa kibaha na kwingineko. Mazao haya vile vile yanaweza yakawa chachu ya kuanzisha viwanda vidogo vodogo vya dawa za miti. Ni mategemeo yangu kuwa wadau wengine kama vile Mamlaka ya Dawa na Chakula ya Wizara ya Afya nayo yatajiunga na mkakati huu ili kuimarisha mafanikio ambayo yanatarajiwa.

Ndugu washiriki, kabla ya kufungua hii warsha naomba niwashukuru waandaaji wa warsha hii pamoja na wachangiaji ambao wamewezesha warsha hii kufanyika. Napenda kuwashukuru pia kwa kuchagua kufanyia mradi huu, na warsha hii katika Mkoa wangu. Hii ni bahati kubwa sana kwa Mkoa wetu tukizingitia kuwa Tanzania ni kubwa na waandaaji wangeweza kwenda sehemu nyingine kufanyia huu mradi. Kwa bahati hii tuliyopata, mimi naomba mzingatie kwa makini sana yale yote mtakayofundishwa kwenye warsha hii na kwenda kuyafanyia kazi huko vijijini kwenu. Mimi binafsi naahidi kufuatilia kilimo cha mimea hiyo na kuona kuwa inatumika vizuri katika kuboresha maisha ya watu wanaoishi na virusi vya UKUMWI na watu wengine ambao wanakabiliwa na matatizo mbalimbali ya lishe kwenye Mkoa wetu. Nitapenda kuona kuwa kilimo hiki kinaenea Mkoa mzima wa Pwani, na kuwezesha uanzishwaji wa viwanda vidogo vidogo vya usindikaji wa haya mazao, kama vile kutengeneza mvinyo wa rosella.

Kwa hayo machache, ninachukua fursa hii kuwatakia mafanikio katika warsha hii, na hasa hasa utekelezwaji wa huu mradi wa miti ya vyanzo vya lishe.

Sasa kwa kuhitimisha ninatamka rasmi kuwa warsha hii imefunguliwa.

UMUHIMU WA LISHE KATIKA KUBORESHA MAISHA YA WATU WANAOISHI NA UKIMWI

DK. GABRIEL T. NDUNGURU

MTAFITI-LISHE

UTANGULIZI

- *Madhara ya ugonjwa wa UKIMWI katika jamii*
    1. *Huua wazalishaji wa chakula*
    2. *Husababisha kero nyingi za utunzaji*
    3. *Huua wafanyakazi*
    4. *Huongeza gharama za matibabu*
    5. *Huathiri elimu*
- *Magonjwa yanayoweza kusababishwa na UKIMWI*

1. Homa za mara kwa mara

2. Kikoozi

3. Mwasho wa mwili

4. Kuharisha sana

5. Pumu

6. TB

7. Vidonda vya mdomoni



Athari za magonjwa mwilini

- *Huongeza mahitaji ya kani (Energy) mwilini*
- *Hupunguza hali ya mwili kufyonza chakula vizuri kutoka tumboni*
- *Uharibu nguvu ya dawa mbalimbali*
- *Husababisha kuharisha*
- *Husababisha magonjwa ya mara kwa mara*
- *Huongeza mahitaji ya viini lishe kwa ujumla*
- *Husababisha chakula kuto tumika vizuri mwilini*
- *Usababisha uvimbe mwilini*

Kazi ya lishe mwilini

- *Kuongeza kinga mwilini*
- *Kuponyesha magonjwa mbalimbali*
- *Kuzuia magonjwa*
- *Kujenga mwili*
- *Kuleta nguvu*

Aina mbalimbali ya vyakula

- *Vyakula vya proteni*
- *Vyakula vya wanga*
- *Vyakula vya mafuta*
- *Vitamini mabalimbali kama vile A, kundi la B, C na E.*
- *Madini mabalimbali kama vile Chuma na zinc*

JUHUDI ZA SERIKALI NA MASHIRIKA YA KIMATAIFA NA KITAIFA

- *Kusambaza dawa ya kuongeza maisha*
- *Kuhamasisha lishe bora*
- *Kupima afya za watu*
- *Kutoa elimu kuhusu UKIMWI*
- *Kufanya utafiti kuhusu UKUMWI*

MALENGO YETU

Kutumia nguvu zetu zote katika kuunga mkono juhudi za serikali kwa:

- *Kutafuta tiba mbadala*
- *Kutafuta mbinu za kuboresha lishe ya watu wanaoishi na virusi vya ukimwi*
- *Kupeana taarifa kuhusu matokeo ya utafiti wetu*
- *Kuzalisha mazao mbalimbali yenye sifa za kutibu magonjwa na kuboresha lishe*

MATUMIZI NA ULIMAJI WA MLONGE

(*Moringa oleifera*)

DR. MAINEN MOSHI

1. UTANGULIZI

- *Mlonge ni Nini?*
- *Mlonge ni mti mdogo, na unaokuwa kwa kasi, unaovumilia ukame*
- *Huweza kufikia kimo cha meta 12 unapokomaa*
- *Hukua sehemu mbalimbali*
- *Una matumizi mbalimbali kwa binadamu na mifugo.*
- *Majani na matunda yana virutubisho vya aina ya protini, vitamini, madini*
- *Mmea huu hutumika kama dawa*

2. Mti wa Mlonge

- *Ni mti laini wenye shina moja, matawi kadhaa na vijani vidogo vidogo*
- *Mizizi yake hujishika vizuri ardhini*
- *Maua yake yana rangi ya maziwa na hutoa harufu nzuri*
- *Matunda yake huwa na urefu wa sm 30-50 na yanafanana na ya kunde*
- *Mbegu zake ni nyeusi na zina "mabawa"*

3. Mahitaji ya Mlonge

- *Hupendelea sehemu zenye mvua za wastani kiasi cha mm 250-1500 kwa mwaka*
- *Pia hustahimili joto na sehemu lowezi zenye mvua zaidi ya mm 3000 kwa mwaka*
- *Huota katika mwinuko wa hadi kufikia meta 1000 kutoka usawa wa bahari*
- *Hupendelea udongo unaopitisha maji kirahisi na usiotuama maji hasa wa mchanga*
- *Tanzania: Unakua vizuri ukanda wa pwani*

4. Ulimaji wa Mlonge

- *Mlonge huweza kuoteshwa kutokana na mbegu au vipandikizi/vijiti*

4.1 Uoteshaji wa mbegu kwenye bustani/shambani

- Loweka mbegu kwenye maji kwa usiku mzima na vunja gamba la mbegu
- Otesha mbegu 2-3 kwenye kikapu (chenye urefu sm 18, upana sm 12) kilichojazwa vizuri na mchanganyiko wa udongo na mchanga (3:1), katika kishimo cha sm 1-2.
- Mbegu huota kati ya siku 5-14

- *Lima ardhi vizuri kabla ya kupanda miche*
- *Chimba mashimo ya upana wa sm 50 na kina sm 50*

- *Changanya kilo 5 za mbolea ya asili na udongo wa juu na weka kwenye shimo la kupandia mti*
- *Ni vizuri kupanda miche wakati wa mvua au weka maji siku moja kabla ya kupanda*

- *Weka maji kidogo siku za mwanzo*
- *Endapo miti itainama ifunge kwenye miti ya urefu wa sm 40 ili kuisaidia*

- *4.2. Upandaji wa mbegu moja kwa moja shambani*
- *Chimba shimo la kutosha kuweka mbolea na kumwagia maji kabla ya kupanda kwenye bustani ya nyumbani wakati wowote ikiwa unaweza kumwagilia*

- *Katika shamba kubwa ni vizuri kupanda mbegu mwanzoni mwa msimu wa mvua*

- *4.3. Upandaji wa vijiti*
- *Tumia vijiti vya mti uliokomaa vilivyokatwa katika vipimo vya urefu sm 45-100 na unene sm 4-10.*
- *Vijiti huweza kupandwa moja kwa moja au kwenye vikapu*
- *4.3.1 Moja kwa moja: Panda kwenye udongo mwepesi wenye kichanga na panda sehemu moja ya tatu ya kijiti chini ya ardhi, mwagilia maji kiasi ili mizizi isioze*
- *4.3.2 Kwenye Vikapu: Unaweza kuongeza mbolea (km phosphorus) ili kuharakisha ukuaji. Vijiti vinaweza kuoteshwa shambani baada ya miezi 2.*

5: Nafasi katika upandaji

- *Panda katika nafasi ya mita 3 kati ya miti na mita 3 kati ya mistari*
- *Panda miti mashariki kuelekea magharibi ili kuruhusu mwanga wa jua na hewa ya kutosha*
- *Miti ya milonge inaweza kuchanganywa na mahindi, ufuta nk baada ya miaka 2.*

6. Ukataji wa ncha za miti

- *Miche ikishafikia urefu wa sm 60 ikatwe kwenye ncha urefu wa sm 10 kutoka juu*
- *Matawi ambayo huota juma moja baada ya kukata ncha yakatwe yakishafikia urefu wa cm 20.*
- *Ukataji wa matawi ufanyike X4 kabla ya miche kutoa maua (miezi 3 hivi) ili kuruhusu mti kuota majani, matawi na matunda mengi*
- *Kwa aina ya miloge mikubwa shina lote likatwe mara moja kwa mwaka katika urefu wa sm 90 kutoka ardhini.*

7. Wadudu na magojwa

- *Milonge huvumilia kushabuliwa na wadudu*
- *Mizizi huweza kushambuliwa na fungua aina na Diplodia kwenye maeneo yanayotuama maji*
- *Miti midogo hushambuliwa na wanyama km ng'ombe, mbuzi, kondoo, nguruwe nk*
- *Ni vyema kupanda miti ya uzio hususani "*Jatropha curcas*" ambayo matunda yake hutengeneza sabuni*
- *Pia miche huweza kushambuliwa na mchwa*
  - Zuia uharibifu huu kwa kuzungushia kwenye shina majani ya mti wa mbono, majani ya mti wa "Tephrosia"; weka jivu kwenye shina

8. Uvunaji

- *Vuna majani machanga na vikonyo kwa ajili ya kuliwa*
- *Vuna majani yaliyokomaa kwa ajili ya kutengeneza unga*
- *Vuna matunda ya mlonge mchanga yenye unene wa sm 1 kwa ajili ya chakula*
- *Mbegu zivunwe kutoka katika tunda lililikomaa na kukauka(linakuwa la rangi ya kahawia)*
- *Mbegu zihifadhiwe kwenye mifuko mikavu na inayoruhusu hewa*

9. Matumizi ya Mlonge

9.1 Matumizi ni mengi:

- *Majani ya mlonge ni chanzo kizuri cha madini ya kalsium, potasiam, chuma, shaba;*
- *Majani yana vitamin A, B and C*
- *Mlonge pia una protein yenye ubora*
- *Matunda pia ni chanzo kizuri cha protini*
- *Mbegu za mlonge hutengeneza mafuta*

9.2 Mlonge ni Dawa!

- *Huweza kutibu magonjwa yanayosababishwa na bakteria, fangasi na virusi*
- *Mizizi: hutibu homa na pumu*
- *Pia hupunguza matatizo katika mfumo wa kukojoa*
- *Majani husaidia uyeyushaji wa chakula tumboni, huzuia vidonda vya tumbo na pia hutibu sikio*
- *Maua: hutibu majipu*
- *Matunda: huongeza hamu ya kula na ni dawa ya macho*
- *Hutibu pia magonjwa ya mfumo wa damu*
- *Mbegu hutoa mafuta kutengenezea sabuni*

10.Hitimisho

- *Mlonge ni zao muhimu .*
- *Ni Dawa na ni chakula*
- *Una Vitamin A ambayo ni muhimu sana kwa watoto*
- *Una madini ya Chuma ambayo ni muhimu kwa watoto na akina mama wajawazito na wanaonyonyesha*
- *Una madini, protini na vitamini ambazo huweza kuongeza kinga ya mwili dhidi ya magonjwa*
- *Huweza kuzuia magonjwa yanayoambukizwa (Kuumwa sikio) na yasiyo ambukizwa (pumu, presha)*
- *Ni zao linaloweza kulimwa na kuchangia katika kuboresha afya na kuongeza kipato!!!*

ULIMAJI NA UTUMIAJI ENDELEVU WA *HIBISCUS SABDARIFFA* – MALVACEAE (ROSELLE)

Mr. Edwin Shunda

Utangulizi

- *Rosella ni mmea wenye virutubisho vingi km vitamini, na madini ya chumvichumvi*
- *Hutumika kutengenezea juisi, jam, jellies, sauces, na mvinyo (pombe)*
- *Hutumika kuukinga mwili na magonjwa km saratani, ini na ukosefu wa lishe*
- *Unapunguza rehamu, unatibu presha*
- *Mmea wa Rosella wenye maua mekundu hujulikana kama choya-Dodoma*
- *Huitwa mkakaka(pwani) na wengine huutumia kama kiungo cha mboga(ndimu)*
- *Majani yake yanaweza kuliwa kama mboga vilevile*
- *Ni zao la biashara na hutumiwa nyumbani*

Mrosela

- *Mmea huu hukua na hufikia urefu wa mita 3.5 kwa msimu*
- *Mti pamoja na matawi yake vimenyooka*
- *Majani yamepishana kimpangilio na kugawanyika katika sehemu 3 – 7 pembeni yakiwa kama msumeno*
- *Una rangi ya kijani, nyeusi hadi nyekundu*
- *Maua ni makubwa yenye rangi nyekundu hadi njano*
- *Una mzizi mrefu na hutoa maua wakati wa kiangazi.*
- *Pia unavumilia ardhi yenye tindikali ya juu na ya chini pamoja na magonjwa*
- *Kuna aina 2:*
  - *Hibiscus sabdariffa* yenye vikonyo vya rangi nyekundu hadi njano ambavyo vinaliwa
  - *Hibiscus altissima* Webster ambayo hupandwa zaidi kwa ajili ya kamba kamba (fibres) zake lakini vikonyo haviliwi

Mahitaji ya Mrosela

- *<u>Hali ya Hewa</u>:*
- *Maeneo ya tropiki yenye mvua kati ya 1500 – 2000 mm kwa mwaka*
- *Mwinuko wa hadi meta 600 kutoka usawa wa bahari*
- *Inavumilia joto na hali ya unyevunyevu*
- *Hupendelea udongo wa mchanga wenye rutuba ambao hupenyeka kwa urahisi*

Mahitaji ya Rosela

- Hata hivyo unaweza kukua kwenye aina mbalimbali za udongo
- *Huhitaji palizi ya mara kwa mara ili kuondoa kivuli na majani*
- *Huvumilia mafuriko, upepo mkali na maji yaliyotuama*

Ulimaji:

- Uchaguzi wa eneo, utayarishaji wa eneo, uchaguzi wa mbegu
- Mahitaji ya bustani : vikapu, mbolea, udongo, mchanga

- *Tifua ardhi vizuri kwenda chini kama sentimeta 20*
- *Piga mashimo ya ukubwa wa sm15 X sm 15 na kina cha sm 5*
- *Panda mbegu kilo 11 – 22 kwa hekta*
- *Ni vyema kupanda mbegu kwa mistari*
- *Palizi katika mwezi wa kwanza ni muhimu sana*
- *Mbolea za asili zinafaa kutumika na husaidia sana*
- *Mtindo wa kubadilisha mazao (crop rotation) hutumika hasa kwa ajili ya mdudu anayeshambulia mmea huu kwenye mizizi (root knot nematode)* Heleredera radicicola
- *Unaweza kubadilisha na mazao ya kijani kama kunde, mahindi*
- *Mashamba madogo nyumbani:*
  - Panda mistari halafu ikisha ota punguza iwe katika mistari ya meta 1 x meta 1.
- *Mashamba makubwa:*
  - Mbegu zioteshwe kwenye kitalu halafu zipandwe shambani kwa upana wa meta1.3 hadi 2.6 na mistari ya upana wa meta 2-3.3

Magonjwa

- *Fungi: fangas (ukungu) mbalimbali hushambulia kwenye mizizi na majani*
  - Nyunyiza dawa, fungicides

Kumbuka: Uangalizi wa shamba unahusisha;

- Palizi, Kukata mapukutu, kufyeka
- Kunyweshea
- Uwekaji mbolea
- Uwekaji dawa kwa wadudu waharibifu

Uvunaji

- *Uvunaji wa matunda na vikonyo hufanyika majuma 3 baada ya maua kuchipua.*
- *Inashauriwa vikonyo viondolewe baada ya kupika matunda*
- *Kwa Rosela ya kamba: kupanda hadi kuvuna ni miezi 3-4 na ivunwe wakati mimea inatoa maua*
  - Mimea ikatwe chini kabisa na kisha kuning'iniza ili kamba ziachane na mti
  - Kamba zioshwe na kuanikwa juani
  - Mashine zipo na zinaweza kutumika kwa ajili ya kutenganisha kamba na mti

- *Ukaushaji Unafanywa kwa kutumia*
  - solar dryer
  - chekecheke
  - Kuanika moja kwa moja juani
  - Kutumia majamvi kwa kukaushia matunda yenye mbegu

Maandalizi:

- *Andaa turubai, jamvi, mkeka nk*
- *Bandua vikonyo*
- *Hifadhi matunda yenye mbegu*

Kuhifadhi

- *Weka rosela iliyokauka kweye mifuko safi ya nailoni au viroba*
- *Hifadhi mifuko kwenye chumba kisafi chenye mzunguko mzuri wa hewa na kisiwe chenye unyevunyevu*

Uvunaji wa kiuchumi

- *Uvunaji wa vikonyo kilo 1.5-7.5 kwa mmea*
- *Kilo 17000-19000 kwa hekta*
- *Uzalishaji wa kamba ni kg 1700 – 3500 kwa hekta*
- *Kiasi cha kamba kwenye rosela ni 5%*

Matumizi ya Rosela

- Majani, matunda, maua, vikonyo, mbegu, mizizi

- *Vikonyo vya matunda hutumika kutengenezea jams, jellies, sauces na mvinyo*
- *Vikonyo pia hutumika kuweka rangi na ladha kwenye vyakula*
- *Majani machanga huliwa kama mboga*
- *Mbegu hutumika kwa ajili ya kuongeza nguvu za kiume*
- *Matunda yake yanaliwa*
- *Kamba zake hutengenezea vitu mbali mbali*
- *Rosela pia hutoa mafuta*

Matumizi kama dawa asilia

- *Huongeza nguvu za kiume*
- *Hutibu magonjwa ya tumbo, majipu, matatizo ya moyo, kikohozi, kansa (vikonyo), homa homa, na magonjwa ya akili*
- *Hupunguza kiwango cha kulewa kwa mtu anapokunywa pombe*
- *Maua yake ni mazuri sana katika kupunguza rehani kwenye damu*

Hitimisho

- *Ni zao lenye matumizi mengi yenye faida*
- *Linaweza kulimwa kama zao la biashara*
- *Linaweza kuongeza ajira*
- *Linaweza kuongeza kipato na kupunguza umasikini*
- *lnatengeneza mvinyo mzuri sana.*

ULIMAJI NA UTUMIAJI ENDELEVU WA *ALOE VERA*

na Dr. Mainen J. Moshi

Utangulizi

- *Aloe vera (*Aloe barbadensis *L.) ni mojawapo ya mimea iliyojulikana zamani kama mimea ya tiba*
- *Inasemekana ulitumika kunakshi mwili wa bwana Yesu Kristo*
- *Kihistoria ni tiba ya kufunga choo, kuungua, vidonda, michubuko, ngozi, figo n.k.*
- *Una aina kadhaa za "amino acids", vimeng'enyo, vitamini na madini*
- *Unaongoza kati ya mimea ijulikanayo kwa kuongeza viini vya uhai kwenye mwili wa mwanadamu!!!*

- *Una uponyaji wa asili na nguvu za kutoa sumu tumboni*
- *Husaidia kuponda chakula kilichoganda na na hulainisha choo*
- *Huzuia kuharisha, na ni kichocheo kwenye mfumo wa kinga, unapunguza maumivi na unaongeza ukuaji wa chembechembe*
- *Una kiasi kikubwa cha viini lishe pamoja na vitamini E, C, B1, 2, 3 na 6 na madini kama Fe, Mn, Ca na Zn.*
- *Huweza kutumika kama lishe mbadala kwa wagonjwa wa ukimwi (HIV/AIDS)*

Ulimaji

- *Unapendelea zaidi udongo wenye mchanga na rutuba ingawa huota ktk aina nyingi za udongo*
- *Huwa unakuzwa kwa kutumia:*
  - maoteo (root suckers)
  - mabaki ya mizizi baada ya kuvuna (rhizome cuttings) ambazo hukatwa sentimeta 5 – 6 urefu na vyenye vijicho (nodes) 2 – 3.
- *Vinapandwa kwenye matuta maalum au vihifadhio*
- *Miche impandwa baada ya kuanza kuchipua*

- *Ulimaji wa Aloe vera unafuata hatua zifuatazo:*
  - Ardhi ilimwe vizuri na udongo uwe na tindikali kiasi; Inashauriwa kuongeza mbolea aina ya ammonium nitrate kila mwaka
  - Miche ipandwe katika umbali wa inchi 31 kati ya mche na mche na kati ya mstari na mstari (heka miche 5,000; na itachukua miezi 18 – 24 kwa majani ya Aloe vera kukomaa)
  - Kwa mwaka mmoja mimea itatoa maua yenye rangi ya njano na majani yenye urefu wa futi 1 hadi 2 hukatwa bila kuharibu mmea ili udumu kwa miaka kadhaa
- *Uvunaji hufanywa mara nne kwa mwaka katika kiwango cha majani kwa kila mmea. Hivyo majani 12 huvunwa kutoka kwenye kila mche*
- *Kwa wastani kila mwaka unaweza kuvuna kg 60,000 kwenye hekari moja*
- *Majani yakishavunwa, mara moja huwekwa kwenye boksi la mbao lililoundwa kama V lenye upana wa futi 4 na kina cha inchi 12 – 18 sehemu iliyokatwa ikielekea chini.*

- *Boksi la mbao huwekwa kwenye mwinuko ambao huruhusu juisi kutoka kwenye majani itiririke haraka na kudondokea kwenye chombo kilichowekwa chini kupitia tundu lililopo kwenye boksi hilo*
- *Majani hayachemshwi bali baadaye hutumika kama mbolea. Maboksi yakishajaa, huondolewa na kuhifadhiwa*
- *Juice huwekwa kwenye chombo cha shaba na kuchemshwa*
- *Sehemu ya chini imetengenezwa ili kuhifadhi takataka ambazo huondolewa mara kwa mara wakati uchemshaji ukiendelea*
- *Baada ya uchemshaji, juisi nzito huwekwa kwenye chombo kikubwa cha gudulia au boksi na kuachwa ipoe.*

Matumizi

(1) Husaidia kuhamasisha na kuimarisha kinga kutokana na kuwepo "mannan polysaccharides"

(2) Husaidia magonjwa ya mafua, kikohozi na "Allergies" kutokana na magnesium lactate and salicylates

(3) Husaidia kama "anti – inflammatory agent", hutibu "arthritis" na kusaidia mzunguko mzuri wa damu kwa ajili ya moyo na mfumo wa akili.

(4) Husaidia kushusha kiasi cha rehamu mwilini; kutokana na polysaccharides zilizomo

(5) Inasaidia kama "antioxidant" hivyo hulinda na kuondoa sumu zisizotakiwa mwilini, kurekebisha msukumo wa damu

(6) Hutibu rheumatism, arthritis, maambukizo ya figo, njia ya mkojo (UTI) na prostate

(7)Hutibu matatizo ya tumbo, kama:

- *vidonda vya tumbo*
- *kulainisha choo*
- *Kupunguza tindikali*
- *husaidia chakula kisagwe vizuri tumboni*
- *vidonda na uvimbe kwenye njia ya haja kubwa (haemorrhoids)*

(8) Hutibu ugonjwa wa ini na kisukari

(9) hutumika kutengenezea dawa za aina mbalimbali za ngozi

Hitimisho

- *Aloe vera ni mmea unaojulikana kote duniani kutokana na matumizi yake mengi*
  - Chanzo cha viinilishe (vitamini, madini)
  - Ina kinga ya mwili
  - Ni tiba kwa magojwa mbalimbali
  - Hutumika kutengenezea vipodozi
- *Ni zao la biashara*
- *Linaweza kuongeza kipato na kuondoa umasikini*
- *Inafaa sana kutumiwa na husaidia wagonjwa wenye upungufu wa kinga mwilini (HIV/AIDS)*

HOTUBA YA KUFUNGA WARSHA YA WADAU WANAOHUSIKA NA MADAWA ZA MITI LISHE WILAYA YA KIBAHA, TAREHE 22/05/2006

Mkurugenzi, Taasisi ya Madawa ya Asilia, Chuo Kikuu Kishiriki cha Sayansi za Tiba, Muhimbili, viongozi wa Wilaya ya Kibaha, Wadau wa dawa za kiasili na washiriki wengine wa warsha.

Ndugu wana warsha, kwanza kabisa napenda niwashukuru waandaaji kwa kunikaribisha kuja kufunga warsha hii. Kwa niaba ya Wilaya yangu napenda kuwapongeza wadau wote kwa moyo wenu wa kujitokeza kwa wingi kuja kuhudhuria warsha hii muhimu.

Ndugu washiriki, nimeelezwa kuwa warsha hii ilikuwa ya siku moja ikijumuisha wadau mbalimbali wanaohusika na matumizi ya bidhaa za misitu katika kupata vyanzo mbadala vya kuimarisha lishe, kutibu magonjwa mbalimbali ya binadamu pamoja na yale yanayoambatana na UKIMWI. Binafsi warsha hii imenifurahisha sana kwa vile imelenga pia katika suala zima la hifadhi ya mazingira na kuondoa umaskini katika jamii yetu.

Ndugu washiriki, mimi nimeambiwa kuwa katika hii siku moja washiriki wameweza kujifunza mambo mengi sana ya manufaa kwao na kwa taifa zima. Nimefahamishwa kuwa mmejifunza masuala ya nafasi ya lishe bora katika kuboresha maisha ya wenzetu wanaoishi na virusi vya UKIMWI, jinsi ya kukuza mlonge, rosella na aloe vera na matumizi yake kama dawa mbadala ya maradhi mbalimbali ya watu hao. Nimeelezwa pia kuwa mmejifunza faida ya mazao haya katika kuboresha lishe na kuboresha mazingira. Mimi naamini kabisa kwamba ujuzi huu mliopata mtakwenda kuutumia kwa vitendo na baada ya muda mfupi mazao haya yataonekana yakishamiri mashambani mwenu. Naomba maafisa wote wa ugani wa kilimo na misitu wawahamasishe wakulima kwa bidii katika kuzalisha mazao haya na kuyatumia ipasavyo. Majani ya mlonge, na rosella ni mboga nzuri tu na zenye virutubisho. Wananchi wasingojee wawauzie watu wengine, anzeni kutumia wenyewe ili na wengine wawaone mnavyofanikiwa wawaige. Baadaye hawa watakuwa ndio wanunuzi wa mazao yenu na hapo ndipo biashara itakapoanzia.

Ndugu washiriki, umuhimu wa warsha hii ni mkubwa sana, tukizingatia umuhimu wa mazao haya katika kupambana na janga hili kubwa la UKIMWI, umaskini na mazingira. Kutokana na umuhimu huo, nawaombeni wote ambao mmepata bahati ya kuhudhuria warsha hii kuyazingatia yale yote mliyojifunza hapa na kuyafanyia kazi kwa vitendo. Nawaombeni pia mjenge mshikamano baina yenu ili kuhakikisha kuwa malengo yenu na yale ya Taifa zima yanafikiwa kama tunavyotarajia. Hata hivyo mnaweza msifanikiwe sana kama hamtashirikiana na Taasisi nyingine, kama vile ile ya Madawa ya Asilia Muhimbili

na ile ya utafiti wa magonjwa Tanzania. Taasisi zingine muhimu ni zile za Chakula na Lishe Tanzania pamoja na ile ya Chakula na Madawa.

Kabla ya kufunga naomba niwapongeze tena wote kwa moyo wenu wa kuja kuhudhiria warsha hii na kuwatakia safari njema vijijini kwenu. Naamini mmehamasika vya kutosha na mtakwenda kueneza yale yote mazuri mliyoyapata kwa wenzenu ambao hawakupata fursa ya kuhudhuria warsha hii.

Kwa hayo machache napenda kutamka kuwa warsha imefungwa.

MAJADILIANO

Wajumbe walipata fursa ya kujadili masuala mbalimbali yaliyotokana na warsha kuhusu tiba za asili kama ifuatavyo.

Mada zilizotolewa:

1. Uwezo wa waganga wa tiba ya asilia.

Waganga wengi walidai kuwa na elimu kubwa pamoja na uzoefu wa miaka mingi katika tiba ya asili. Kwa mfano baadhi ya waganga walidai kuwa na uwezo mkubwa wa kutibu maradhi ya shinikizo la damu, kisukari, tumbo na matatizo ya njia ya mkojo. Pamoja na hayo walidai pia kuwa na uwezo mkubwa wa kuwasaidia akina mama wajawazito wenye matatizo ya kujifungua. Baadhi ya akina mama hao ni wale ambao madaktari walionyesha kukata tamaa katika akina mama hao kujifungua salama. Waganga hao walidai kuwa kuwa walikuwa na dawa nzuri za kufunga kizazi na kuondoa ugumba. Waganga walidai kuwa walikuwa na dawa nzuri sana za kuamsha nguvu za kiume.

2. Soko la dawa na bidhaa zingine zitokanazo na miti ya kisili

Waganga walionyesha wasiwasi wao kuhusu soko la dawa zao. Walidai kuwa wanayo mimea mingi majumbani mwao kama vile mlonge, rosella n.k lakini hawajui soko la bidhaa zinazotokana na mimea hiyo. Kwa hivi walishindwa kuona umuhimu wa kuendelea kulima bidhaa hizo.

Mkurugenzi wa Taasisi ya Tiba ya Asili, Muhimbili, aliwahakikishia wajumbe kuwa soko lipo na ni kubwa. Aliwaelimisha kwa kusema kuwa soko la kwanza na kubwa ni sisi wenyewe. Sisi wenyewe tuna mahitaji makubwa sana ya kutumia bidhaa hizo ili kukidhi matatizo yetu ya kiafya. Dawa hizi zinaweza kuuzwa kwa bei nzuri kutokana na mahitaji makubwa. Wasiwasi ulijitokeza kwamba wazalishaji wa bidhaa hizo unaweza kuwa mdogo kuliko mahitaji yake.

3. Haki Miliki ya bidhaa zao.

Wajumbe walionyesha wasiwasi mkubwa wa kupoteza haki zao za kumiliki bidhaa zao endepo watawashirikisha watu mbalimbali katika utengenezaji wa bidhaa hizo. Walionyesha hofu kuwa ya kuibiwa utalamu wao na wao kubaki bila kitu.

Katika kuwatoa hofu waganga hao Mkurugenzi aliwahakikishia kuwa taratibu za kisheria zipo ambazo zinaweza kuwalinda. Taasisi inautaratibu wa kuwekeana mikataba ya kulinda haki miliki na watu ambao inashirikiana nao katika tiba ya asili. Taasisi pia inashirikiana na mwanasheria wa serikali pamoja na wanasheria wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam katika kulinda miliki za watu hao. Kwa hali aliwasihi waganga hao kushirikiana na Taasisi hiyo katika shughuli zao za tiba pamoja kujiunga na chama cha waganga wa tiba ya asili Tanzania.

4. Utunzaji na kuweka kumbukumbu

Katika warsha hiyo ilionekana kuwa waganga wengi wanatibu wagonjwa bila kuweka kumbukumba na kushirikiana na wataalamu wa afya. Hali hiyo ilileta utata wa kuelewa kama kweli dawa husika inauwezo kweli wa kutibu ugonjwa fulani ambao hakuthibitishwa na wataalamu wa afya. Hii pia inaleta ugumu katika kufuatilia maendeleo ya mgonjwa husika.

Waganga walishauriwa kuweka kushirikiana na wataalamu wa afya ili kujua kikamilifu kuhusu aina ya ugonjwa wanaotibu. Kwa hali hiyo walishauriwa kuwapeleka wagonjwa wao kwenye vipimo mbalimabali ili kuona maendelea yao wakati wote wa tiba yao.

Walishauriwa pia kuweka kumbukumbu za tiba zinazoonyesha vipimo vya hospitali, sehemu anakoishi na mfumo mzima wa tiba yake ili kubaini uwezo wa aina za dawa au tiba anayopata.

5. Lishe Bora

Wajumbe walikubaliana kuwa lishe bora ni msingi wa tiba za maradhi yote. Waganga walishauriwa kulipa kipaombele suala la lishe na kuwashauri wagonjwa juu ya umuhimu wa lishe bora. Waganga walikubali kuwa miti mingi ya tiba, pia ina viini lishe kwa wingi ambavyo vinaweza kutumika katika kuboresha afya za wagonjwa.

6. Dawa ya kufunga kizazi

Baadhi ya wajumbe walipendekeza kuwa waganga wajitahidi kutafuta dawa ya kuzuia mimba ili kuondokana na tatizo la kutumia dawa za hospitali ambazo walidai kuwa zina madhara.

Waganga walidai kuwa dawa hizi zipo na zinatumika. Lakini ilikuwa vigumu kuelwa suala hili kwa vile hakuna mifano mingi iliyotolewa kuhusiana na madai hayo.

7. Mbegu za Mlonge, Rossella an Aloe vera

Wajumbe waliiomba Taasisi kuzalisha mbegu za mimea hiyo kwa wingi na kuzigawa kwa wajumbe ili ziweze kupandwa mashambani mwao kwa wingi. Wajumbe walishauri pia maofisa ugani wa kilimo na mali ya asili wahusike kikamilifu katika kusaidia kilimo hiki.

8. Waganga kuvaa mavazi rasmi

Wajumbe hawakuona umuhimu wa kuvaa mavazi ya jadi wakati wa tiba usika. Warsha ilikubaliana kuwa kulikuwa na umuhimu wa kuvaa nguo safi na yenye heshima wakati wa tiba. Sare pia zingefaa kuvaliwa wakati huo kama vile wataalamu wa afya wanavyovaa.

9. Ufafanuzi

Wajumbe walielimishwa pia tofauti kati ya waganga wa jadi na wale wa tiba ya asili. Katika maelezo ya msingi ilionekana kuwa waganga wa jadi bado wana matatizo ya kuhusisha tiba yao na utamaduni wao kama vile mizimu na kupiga ramli.

Waganga wa tiba ya asili ni wazuri kwa vile wanatumia miti na bayonohai katika tiba zao.

MAHUDHURIO

	NAME (JINA)	ANUANI	SAA
1	Albert Budondi	Box 31579 DSM	2.00
2	Angella Tarimo	Box 1984 Dsm	9.26
3.	Margareth Katanga	Box 1984 Dsm	9.26
4	Selina William	Vikuge Kibaha	2.15
5	Omari Shabani	Soga Kibaha	2 15
6	Kashinde Maonaje	Soga kibaha	2 15
7.	SAIDI. A. CHANZI	SOGA	2 - 15
8	[illegible] K. [illegible]	[illegible]	2 . 15
9	Abdalla S. Mpendu	Fosta Misitu	2 . 15
10	COSTANCIA SOLOMON	KIBAHA	2. 15
	CLEOPHA SHEMBILU	BOX 30072 KIBAHA	2. 15
13	OMARY KIHANGA Mganga wa Tiba	PO BOX [illegible]	2.15
14	HALIYAX KIBAYU Mkunga wa Jadi	VIKUGE	2.15
15	KHDIJA ABDALLA MNGAGA ASILI	087-14776 Kongowe	2.15
16	ASHA ATHMANI Mkunga wa jadi	SOGA	2.15
17	ASHA SELEMA JUMA MNGAGA ASILI	0744,899557 Kongowe	2.15
18	SALMA CHUMA MKUNGA WA JADI	SOGA KIBAHA	2 . 15
19	TAGU H. IDD Afisa Mtendaji wa Kijiji - Vikuhe	0748-524263	2 15
20	Asha Bufu - Mkunga wa Jadi	Mjumbe Saba	2.00

	NAME (JINA)	ADDRES ANUANI	TIME SAA	DA TA
21	IDDI DIWANI M/KITI S/MIAA-MISUGUSU	30,22 KIBAHA 0744 436264	8:55 am	22/
22	HAMIS SIMBA	0741-324139		
23	PATRICK B.K. MATEMBELE MGANGA WAJADI	30,000-KIBAHA 0744 995479	"	22/05
24	SAUDA HADIJA MPONDA MKUNGA WA JADI	30,000-KIBAHA	"	"
25	ENNE S. HAULE MKULIMA MISITU	30823-Msangani		"
26	MIKIDADI SULTAN K. SOGA MGA WA JADI		=	-
27	IEZEKIEL SHIGALU	~~MKULIMA~~		
28	MKULIMA MISITU	P.O.BOX 30800		
29	Rajabu N-Kibaya	Mkuti wa	Miaa Kanga	
30	Rajabu I. Simba	I. Mganga	wa	22/5
31	GERSON SILAS	K/KIBAHA		
32	J. G. MWAKA	KILIMO/MIFUGO (W)		22/05
33	KAIM LIAME	Kongowe		
34	R. KAMBI	Kongowe		
35	KASSIM MWINJIMVUA	MLEMBESABA		
36	KASSIM MPATE	VIKOGE	=	K.B
37	JOSEPH H. BUTABU	KONGOWE		JOS
38	HASSAN KIWANITE	KONGOWE	819202	
39	MOHAMMED SALUM	Kongowe		22/5
40	SUFIANI KINDUMBILI	KONGOWE		22/05
41	Zahiri Msangi	Ruvu Forest project Box 30072 Kibaha Simu # 804928		

NAME (JINA)	ADDRES ANUANI	TIM SAA
42 ✓ ZELINA NJAU	30011 KONGOWE	"
43 ✓ ADAMSON D. MWANDALIMA	30011 KONGOWE	"
44 ✓ Lucas Fidelis	30072 "	"
✓ Simon Haule	Mwesagani	"
45 ✓ NOURMUHAMED A REHMAN	—	"
46 ✓ Emmanuel JAPINA	30072	"
* 47 Raymond Mlelwa	2340 DAR	"
* 48 David W. YONAZA	30153 KIBAHA	"
49 RAMADHANI H. BOGHSI	29000 VISIGA	"
50 SAIDI M. MTONDA	0745-891820	"
51 Alex B. MWASINGO	0748-382651	"
52 ALLY SIMBA	0744-810269	"
✓ 53 NASSORO S. A. KAZAMBO	0787-722699	"
✓ 54 HALIMA RASHID TENGWE	—	"
✓ 55 BUSHIRI MPAHAMBO	0746-239764	"
✓ 56 Serafina JOSEPH	30072	"
✓ 57 IBRAHIMU MWALIM	0743-151331	"
✓ 58 SALAMA RAJABU	30072	"
* 59 ZAUDA MPONDA	MISUGUSUGU	"
✓ 60 Paulo Shinda	30072	"
✓ 61 MWAMVITA MUSSA	30072	"
62 MWANJAA MIRAJ.	30072	"
* 63 Ben Komba	0744899621	"
* 64 Magreth Malisa	0745571227	"
✓ 65 Habibu		
✓ 67 Kingi		

Three thousand each participant [signature] 22/5/08

NAME (JINA)	ADDRESS / ANUANI	TIME / SAA	DATE / TAREHE
68 Msangi Zahir	10000/= Each participant		
69 Bugando Katwale			
70 Raymond ~~Katwale~~			
71 Ndozi			
72 Bundondi Albert.		22/3/06.	
73 Komba			
74 Melisa.			
75 Faluma			
76 Margaret Kitange			
77 Angela Tanino			
	Received 90000/= 22/3/06.		
Resource person			Facilitator
Edwin Shunda	40,000/=		
Dr. M. Moshi	40,000/=		
Dr. E. J. Kayombo	40,000/=		
Dr. G. Ndumgwa	40,000/=		
Dr. Z. Mbwambo	40,000/=		
~~Areva M. Mtenga~~ ~~Areva~~.			
Dr. Ndumgwa (workshop preparation)	30,000/=		
Dr. Pax J. Masimba (workshop preparation)	30,000/=		

Mahudhurio

NO	JINA	ANWANI	KAZI	MAHALI UTOKAPO	SAA	TAREHE
1	QUEEN L. MGONDE	~~Box~~ C 787 215052	MSINDIKAJI JINA MSHO NAJI-KITO (NET GROUP)	MKOANI BL/B	3:00	22/5/2006
2	Asha Jumapili	0744 073984	Usindikaji na kutengeneza nguo batiki (KIFONET GROUP)	Mkoani BL/B	3:00	22/5/2006
3	MARY SHAKA	0744 073984	MSINDIKAJI NA KUTENGENEZA NGUO ZA BATIK (KIFONET GROUP)	MKOANI BLK/B	3.50	22/5/2006
4	PRISCA SWAI	Box 30112	A. MTENDAJI KATA KONGOWE	P/NDEGE	3.59	22/05/2006
5	T.G. NWAKA	BOX 3003	KNY AFISA KILIMO/MIFUGO	KIBAHA (W)	3.59	22/05/06
6	HABIB ATHUMANI	Box	MKULIMA	KONGOWE	3.59	22/05/06
7	[illegible]	[illegible]	[illegible]	[illegible]		
8	James P. Nonga	[illegible]	[illegible]			
9	NICEPHORY MNAMBA	Box 30153 KIBAHA	AFISA MTENDAJI WA KATA	SOGA	6.30	22/05/2006

Paid 3000/ each participant 22/5/06

Drewa

M. muya 10,000/=

Kaloli Mos 10,000/=

Secretary

B. Tewba 20,000/=

Wageni waliokuja kufunga na ~~mkutano~~ ~~wa~~ Semina

Mr. Edward Shilogile 50,000/=

mkuu wa mkoa

MS 50,000/=

mkuu wa wilaya)